








Neno	Maana	Picha
<b>Kukata kiungo</b>	Kupoteza sehemu ya mwili, kwa mfano mguu au mkono	
<b>Maumivu kwenye maungio ya viungo viwili</b>	Tatizo la kiafya, ambapo sehemu za maungio ya mtu zinakuwa ngumu na kuvimba na/ au kuwa na maumivu wakati mtu anapojaribu kuziinua.	
<b>Mtindio wa Ubongo</b>	Ni maradhi ambayo yanaweza kuathiri uwezo wa kusogea, nguvu ya misuli, utengamo na uwezo wa kukaa vizuri. Mtindio wa ubongo ni matokeo ya ubongo kupata madhara kabla, wakati au baada ya mtoto kuzaliwa.	
<b>Ugonjwa wa kisukari</b>	Ugonjwa ambao unaambatana na mtu kuwa na sukari nyingi kwenye damu. Hii inaweza kusababisha matatizo ya kiafya ikiwemo; kutokuwa na hisia kwenye sehemu za mwili ( kwa mfano kwenye miguu) na vidonda kwenye shemu za kukanyagia za mtu, kupoteza uwezo wa kuona, kuharibika kwa figo, kupata ugumu kwenye kudhibiti mkojo na kukumbuka vitu kwa taabu.	
<b>Kidonda sehemu ya kukanyagia ya mguu</b>	Ngozi ya sehemu ya kukanyagia ya mguu kukatika katika. Vidonda vya mguu vinatokana na madhara yatokanayo na ugonjwa wa kisukari. Kama vidonda vya kwenye sehemu ya kutembelea ya mguu havijatibiwa; inaweza kupelekea mguu kukatwa. Aidha, vindonda vya kwenye sehemu ya mguu vinitwa michubuko ya sehemu ya kutembelea ya mguu	
<b>Chuma cha kushikiria</b>	Chuma kilicho kwenye ukuta ambachomtu anaweza kushikiria ili kumsaida kusogea.	
<b>Kuwa imara</b>	Kuwa na afya njema na nguvu	
<b>Udhaifu</b>	Hii ni kutokuwa na nguvu, kuumia kwa urahisi au kuwa na nguvu kidogo. Hutokea pale mtu anapokuwa kiumri na afya inapoanza kudorora.	
<b>Orthosis</b>	Ni kifaa ambacho kinamsaidia mtu kusimama. Kinaweza kupunguza maumivu, au kumsaidia kutembea, au kuacha kutokufanya kuzunguka bila ya kutaka.	

<b>Kupooza</b>	Kutokuwa na uwezo wa kusogeza sehemu ya mwili (mara nyingi miguu au mikono).	
<b>Polio</b>	Ni ugonjwa mbaya ambao unasababisha misuli ya mgonjwa inakosa nguvu au inapooza. Hii inaathiri uwezo wa kutoka eneo moja hadi jingine hata baada ya kuona maradhi.	
<b>Kidonda mgandamizo</b>	Kidonda mgandamizo kinatokana na kuharibika kwa ngozi chini ya kidondoa. Hii inatokea kwenye eneo lenye mfupa na inatokea mara nyingi kwa watu wenye matatizo ya hisia au wanaoweza kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa taabu.	

<b>Kiungo bandia</b>	Kiungo bandia ambacho kinachukua nafasi ya kiungo cha mwili kinachokosekana (kwa mfano: mguu)	
<b>Rolata</b>	Kifaa cha kutembelea chenye magurudumu manne.	
<b>Kujitunza</b>	Kuitunza kunamaanisha kuhakikisha unakuwa na afya njema. TAP inafanya shughuli za kujitunza ambazo mtu anafanya kila siku ili kupata mahitaji muhimu. Kwa mafno: kuosha nguo, kwenda chooni, kuvaa nguo, kula na kunywa.	
<b>Hisia</b>	Uwezo wa kuhisi, mgandamizo na maumivu	
<b>Jeraha kwenye uti wa mgongo</b>		
<b>Kiharusi</b>	Damu kutokuweza kufika kwenye ubongo. Hii inaweza kusababisha sehemu ya mwili kukosa nguvu au kupooza pamoja na kuongea kwa taabu, kuhisi kwa taabu, kufikiria kwa taabu na kuona kwa taabu.	
<b>Kisiki</b>	Kiungo cha mwili kinachobaki baada ya kiungo kingine kukatwa mfano sehemu ya mkono au mguu inayobaki inaitwa kingo kilichobaki au kinajulikana zaidi kama kisiki.	
<b>Viatu tiba</b>	Viatu ambavyo vina vitu vinavyosaidia kulinda mguu na kusaidia sehemu ya kutembelea ya mguu ambao uko katika hatari ya kupata kidonda.	
<b>Kuhama</b>	Kusogeza mwili kutoka sehemu moja kwenda nyingine.	
<b>Uwezo wa kubeba mwili</b>	Kiwango cha uzito ambacho mtu anaweza kubeba kwa m(i)guu yake..	